

# eGA yazitaka taasisi za umma kujiunga na mfumo wa GovESB

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imezisisitiza taasisi za umma kujiunga na mfumo wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GovESB) utakaorahisisha kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali ili kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati.

Meneja Mawasiliano wa e-GA, Subira Kaswaga, alitoa rai hiyo jana katika maonesho ya Nanenane jijini Mbeya.


Alisema mfumo wa GovESB ni shirikishi na unawezesha taasisi za umma kuunganisha mifumo yao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuitia mfumo huo ili kuzungumza na kubadilishana taarifa kidijitali.

Alibainisha faida za mfumo huo ni pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma, kuokoa muda, gharama za uendeshaji wa taasisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa wakati.

“Mfumo wa GovESB ni jitihada za mamlaka za kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inazungumza na kubadilishana taarifa ili kupunguza urudufu wa mifumo serikalini.

“Kwa sasa, taasisi mbalimbali za umma zimeunganisha mifumo yake na GovESB lakini zipo taasisi ambazo bado hazijaunganisha, hivyo nitoe wito kwa taasisi hizo kujiunga na mfumo huu wa GovESB,” alisema Kaswaga.

Ofisa TEHAMA wa e-GA, Caesar Mwambani, alisema kuwa mamlaka hiyo kwa kushirikiana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetengeneza mfumo wa e-Mrejesho unaowaweza wananchi kuwasiliana na serikali kidijitali.



**Mfumo wa GovESB ni jitihada za mamlaka za kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inazungumza na kubadilishana taarifa ili kupunguza urudufu wa mifumo serikalini.**